JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# MWONGOZO WA UDHIBITI WA TAKA NGUMU KWA KUTUMIA DHANA YA PUNGUZA, TUMIA TENA NA REJELEZA



*Septemba, 2021*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# MWONGOZO WA UDHIBITI WA TAKA NGUMU KWA KUTUMIA DHANA YA PUNGUZA, TUMIA TENA NA REJELEZA

**Septemba, 2021**

# DIBAJI

Maendeleo endelevu na ustawi wa jamii unapaswa kuzingatia uwepo wa mazingira safi na salama kwa jamii yote. Uchafuzi wa mazingira ni moja ya changamoto kubwa katika uhifadhi wa mazingira hapa nchini, sehemu kubwa ya uchafuzi huu huchangiwa na udhibiti usio endelevu wa taka ngumu. Aidha, uzalishaji wa taka ngumu nchini kwa sasa, unakadiriwa kufikia takriban tani 17.4 milioni za taka kwa siku. Hali hii imechangiwa zaidi na ongezeko la idadi ya watu na kukua kwa shughuli za kiuchumi. Tafiti mbalimbali zinaonesha zaidi ya asilimia 70 ya bajeti za usimamizi na udhibiti wa taka ngumu katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania hutumika katika kukusanya na kusafirisha taka. Kutokana na gharama hizi kuwa kubwa, Mamlaka za usimamizi zimeshindwa kusimamia na kudhibiti taka na hivyo kusababisha taka nyingi kutupwa kiholela katika maeneo yasiyo rasmi.

Hali hii imesababisha kuwepo kwa miji michafu, milipuko ya magonjwa, uharibifu wa mazingira  na miundombinu ikiwemo kujaa kwa taka katika mifumo ya maji taka na mifereji ya maji ya mvua, uchafuzi wa vyanzo vya maji ikiwemo mito, mabwawa na bahari. Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 85 ya taka zinazoingia baharini zinatoka katika maeneo ya nchi kavu yaliyoshindwa kudhibiti taka. Aidha, uwepo wa taka katika bahari na maeneo mengine husababisha vifo na kuathirika kwa viumbe hai ikiwemo mimea, samaki na wanyama wengine.

Ili kukabiliana na changamoto hizi ikiwemo gharama za kusafirisha taka kwenda dampo, Sheria ya Usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004; Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009; na Kanuni za Usimamizi wa Taka ngumu za mwaka 2009 zinaelekeza kuwa uzalishaji wa taka unapaswa kupunguzwa kadri inavyowezekana

ili kuchangia katika kupunguza kiasi cha taka kinachosafirishwa kwenda katika madampo.

Utekelezaji wa matakwa ya Sheria na kanuni za udhibiti taka ngumu utafanyika kwa kutumia mfumo wa Punguza, Tumia Tena na Rejeleza (PTR) taka unaotambulika zaidi kama 3R yaani *Reduce, Re-use and Recycle* kwa lengo la kuimarisha udhibiti na usimamizi endelevu wa taka ngumu nchini. Hivyo serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa mwongozo wa Punguza, Tumia tena na Rejeleza ambao unaendana na matakwa ya sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka, 2004 na Kanuni ya Usimamizi wa Taka Ngumu ya Mwaka 2009 zinazohimiza juu upunguzaji wa kiasi cha taka kinachozalishwa kabla ya kupelekwa dampo. Aidha, Mwongozo huu umebainisha hatua kwa hatua shughuli zinazopaswa kutekelezwa na wadau mbalimbali katika kufanikisha utekelezaji wa dhana ya hii. Vilevile Mwongozo huu unalenga: Kutoa maelekezo ya kutekeleza dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza katika usimamizi na udhibiti wa taka ngumu nchini; Kuwezesha jamii kupata kipato kupitia shughuli za urejelezaji; Kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya Sheria na kanuni, hususan katika kutekeleza taratibu za kupunguza, kutumia tena, na kurejeleza taka ngumu; na Kukuza uelewa wa wadau katika kutekeleza majukumu yao ili kufanikisha usimamizi na udhibiti wa taka ngumu.

Kwa muktadha huo, ni matumaini yangu kwamba utekelezaji wa Mwongozo huu utachangia katika uboreshaji wa usafi wa mazingira, kukuza uelewa, kuongeza kipato kwa jamii na kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za udhibiti na usimamizi wa taka ngumu nchini.

Hivyo, ninachukua fursa hii kuwaomba wadau wote nchini kutumia Mwongozo huu katika kuwezesha shughuli za udhibiti

wa taka nchini kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza.

Selemani Said Jafo (Mb.)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA**

# SHUKRANI

Kukamilika kwa Mwongozo huu wa Usimamizi na Udhibiti wa Taka ngumu kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza ni matokeo ya jitihada za dhati za wadau mbalimbali wa usimamizi na udhibiti wa taka ngumu nchini.

Aidha, ni matumaini yangu kuwa mafanikio ya utekelezaji wa Mwongozo huu, unahitaji ushiriki mkubwa wa wadau wote waliopo katika mnyororo wa udhibiti wa taka. Wadau wanaolengwa katika utekelezaji wa Mwongozo huu ni pamoja na maeneo ya biashara; Taasisi na idara za Serikali; Taasisi za elimu; Viwanda; Sekta ya ujenzi; Sekta ya afya na Jamii kwa ujumla.

Napenda kutoa shukrani kwa timu ya wataalamu iliyoshiriki katika kuandaa Mwongozo huu. Timu hii iliundwa na wataalamu kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Viwanda na Biashara; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Halmashauri za Majiji ya: Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza yalitumika kuwakilisha Halmashauri zote nchini.

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Bw. Mohammed Khamis Abdulla, Naibu Katibu Mkuu, OMR na Dkt. Andrew M. Komba, Mkurugenzi wa Mazingira kwa kushirikiana kusimamia na kuratibu maandalizi ya Mwongozo huu. Vilevile napenda kutoa shukrani kwa menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Mwongozo huu.

Mwisho, nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao

kwa namna moja ama nyingine katika kuandaa Mwongozo huu uliokusudia kuweka mfumo utakaowezesha kupunguza uzalishaji taka, kuhamasisha urejelezaji na matumizi mbadala ya taka.

Mary N. Maganga
**KATIBU MKUU**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# TAFSIRI YA MANENO NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **Kanzidata** | Mfumo maalumu wa kielektroniki unaotumika kuhifadhi taarifa |
| **Malighafi** | Taka zinazotumika katika kutengeneza bidhaa |
| **Maeneo ya Biashara** | Masoko, maduka makubwa na madogo, Maghala, Karakana, Kantini, Migahawa, Hoteli na nyumba za kulala wageni. |
| **Maeneo ya Kutoa huduma za Afya** | Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali |
| **Maeneo ya Makazi** | Maeneo ambayo watu wanaishi |
| **Mboji** | Mbolea itokanayo na taka zinazooza |
| **PTR** | Punguza, Tumia tena na Rejeleza |
| **Taasisi** | Wizara, Wakala na Idara za Serikali, Taasisi Binafsi |
| **Taasisi za Elimu** | Shule za Awali, Msingi, Sekondari; na Vyuo vya Elimu ya Kati na Juu |
| **Taka Ngumu** | Taka za mabaki ya vyakula, chupa za kioo na plastiki, chuma, mbao, nguo, majani. |
| **Viwanda** | Maeneo maalum yanayochakata malighafi kutengeneza bidhaa nyingine |
| **Warejelezaji wa Taka** | Kampuni, kiwanda au watu binafsi wanaojihusisha na kuchakata taka kwa ajili ya kutengeneza bidhaa. |
| **Watoa huduma ya uzoaji wa taka** | Makampuni au vikundi vinavyoingia Mkataba na Taasisi au Halmashauri kwa ajili ya kuzoa taka katika maeneo yao |
| **Wazabuni** | Watoa huduma ya bidhaa kwa viwanda au makampuni |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Hali ya Usimamizi na Udhibiti wa Taka ngumu Nchini

Tanzania kama zilivyo nchi nyingi kusini mwa Jangwa la Sahara, imeendelea kushuhudia ongezeko la uzalishaji wa taka linalosababishwa na ongezeko la watu mijini. Takwimu zinaonesha idadi ya watu waishio mijini nchini Tanzania iliongezeka kutoka 617,500 mwaka 1967 hadi kufikia 13,691,550 mwaka 2012. Ongezeko hili limeambatana na changamoto mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa uzalishaji wa taka. Kiwango cha uzalishaji wa taka nchini kinakadiriwa kufikia tani milioni 17.4 kwa mwaka 2019 (VPO, 2019a).

Hata hivyo hali ya ukusanyaji na utupaji salama wa taka katika miji mbalimbali nchini imekuwa si ya kuridhisha. Kwa mfano, Jiji la Dar es Salaam hukusanya takribani asilimia 50 tu ya kiasi cha tani 5,300 zinazozalishwa kwa siku wakati Jiji la Arusha hukusanya kiasi cha asilimia 54.8 ya kiasi cha tani 550 zinazozalishwa kwa siku na Jiji la Mbeya hukusanya asilimia 35 ya kiasi cha tani 400 zinazozalishwa kwa siku. Vilevile jiji la Mwanza hukusanya asilimia 67.2 ya kiasi cha tani 338 zinazozalishwa kwa siku na Jiji la Dodoma hukusanya asilimia 33 ya tani 305 zinazozalishwa kwa siku. Hali hiyo inasababisha wastani wa asilimia 50 ya taka zinazozalishwa kubaki katika mazingira ya Majiji na Miji mbalimbali nchini na hatimaye kusababisha madhara kwenye jamii ikiwemo milipuko ya magonjwa kama vile kipindupindu, homa ya matumbo, kuharisha nk.; kuharibika kwa mandhari kutokana na kuenea kwa taka kwenye maeneo mbalimbali kama

vile kando kando ya barabara, kwenye maeneo ya wazi, kwenye Mito na fukwe za Bahari na Maziwa; Kuharibika kwa mifumo ikolojia ya maeneo mbalimbali kama vile baharini, kwenye maziwa na mito; na uharibifu wa miundombinu unaotokana na mafuriko yanayosababishwa na kuziba kwa mfereji ya maji ya mvua kwa sababu ya utupaji taka usio salama.

Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa Miji/Majiji katika nchi nyingi zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania hutumia zaidi ya asilimia 70 ya bajeti ya usimamizi na udhibiti wa taka ngumu kwa mwaka kwa ajili ya kukusanya na kusafirisha taka pekee. Hali hii inasababisha mamlaka za Serikali za Mitaa katika nchini nyingi ikiwemo Tanzania kushindwa kumudu gharama za udhibiti wa taka ngumu na hivyo kiasi kikubwa cha taka kutupwa katika maeneo yasiyo rasmi kama vile mito, maeneo ya wazi na mifereji ya maji ya mvua.

Jitihada za kukabiliana na changamoto ya gharama kubwa za kusafirisha taka kwenda dampo, zinapaswa kuendana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004; Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 na Kanuni za usimamizi wa Taka Ngumu ya mwaka 2009 ambazo zinaelekeza wajibu wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha uzalishaji wa taka unapunguzwa katika maeneo yao. Aidha mwongozo wa Punguza, Tumia Tena na Rejeleza (PTR) unalenga katika kuweka mfumo wa kitaasisi wa Udhibiti wa Taka ngumu kwa kupunguza gharama za usimamizi na uendeshaji kwa kushirikisha wadau wote muhimu katika shughuli za udhibiti wa taka ngumu.

## 1.2 Changamoto zilizopo katika usimamizi wa Taka ngumu

Mfumo wa usimamizi wa taka unaotumika kwa sasa nchini unahusisha ukusanyaji na upelekaji wa taka moja kwa moja dampo. Aidha, tafiti mbalimbali zinaonesha mfumo huu umeshindwa kuleta ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa taka ngumu. Hii inatokana na ukweli kwamba mamlaka nyingi za serikali za Mitaa nchini zinakabaliwa na changamoto mbalimbali kama vile kukosekana kwa maeneo ya kuhifadhi taka kwa muda (*waste transfer stations*); umbali mrefu kwenda dampo; uhaba wa magari ya taka; ufinyu wa bajeti na uhaba wa zana na vifaa vinavyotumika katika udhibiti wa taka ngumu. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa gharama za usimamizi na udhibiti wa taka ngumu na hivyo kiasi cha taka kinachokusanywa na kupelekwa dampo kuwa chini ya aslimia 50 katika maeneo mengi nchini. Baadhi ya watafiti akiwemo Visvanathan (2007), Seow (2017) and Yhdego (2018) wameeleza kwamba mfumo wa Punguza, Tumia tena na Rejeleza kuwa ndiyo mfumo unaofaa katika kukabiliana na changamoto za usimamizi na udhibiti wa taka ngumu mijini. Aidha tathmini iliyofanyika katika nchi zaidi za Korea, Taiwan, Singapore, Hongkong na Japan Mfumo huu unapunguza kiasi cha taka kinachopaswa kwenda dampo na hivyo kupunguza gharama za udhibiti wa taka ngumu hasa usafirishaji wa taka kwenda dampo ambao unakadiriwa kutumia wastani wa asilimia 70 ya bajeti ya udhibiti wa taka ngumu.

## 1.3 Umuhimu wa Mwongozo wa PTR

Kuongezeka kwa uzalishaji wa taka; kiasi kidogo cha bajeti kinachotengwa na mamlaka za Serikali za Mitaa katika usimazi na udhibiti wa taka ngumu; gharama kubwa za usafirishaji wa taka kwenda dampo na kukosekana kwa rasilimali fedha kwa ajili

ya ujenzi wa madampo ya kisasa kunapelekea umuhimu mkubwa wa kupunguza kiasi cha taka kinachozalishwa. Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira imeandaa mwongozo huu ili kuwezesha wadau wa usimamizi na udhibiti wa taka kutekeleza matakwa ya kisheria katika kupunguza kiasi cha taka kinachopelekwa kwenye madampo. Mwongozo huu unalenga kuwezesha utekelezaji wa dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza (PTR) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika udhibiti wa taka ngumu nchini. Kifungu cha 55 (g) cha sheria za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kinaelekeza jukumu la usimamizi wa udhibiti wa taka ngumu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo pamoja na kwamba mamlaka za Serikali za Mitaa kupewa jukumu hilo kisheria, na kuwepo kwa sheria na kanuni za udhibiti wa taka bado hakukuwepo mwongozo unaoelekeza utaratibu, hatua na mbinu zinazopaswa kufuatwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine ili kutekeleza mpango wa kupunguza uzalishaji wa taka.

# SURA YA PILI

# 2.0 HALI HALISI

## 2.1 Ukubwa wa Tatizo la udhibiti wa Taka ngumu nchini

Tanzania kama zilivyo nchi nyingi kusini mwa Jangwa la Sahara huduma ya udhibiti wa taka ngumu imekuwa si ya kuridhisha (Omar, 2019; Omar, 2020 and Omar, 2021). Kiasi cha taka kinachokusanywa kwa siku katika miji mingi kimeendelea kuwa chini ya asilimia 50. Hali hii imesababisha taka kudhibitiwa katika njia zisizo salama ambapo takribani asilimia 3 ya taka zinazozalishwa huchomwa kiholela, asilimia 30 hufukiwa, na asilimia 17 hutupwa hovyo katika mazingira ikiwemo maeneo ya wazi, mifereji ya maji ya mvua na vyanzo vya maji kama vile mito, maziwa, na bahari.





*Kielelezo Na. 1: Taka zikitupwa katika Mto Msimbazi eneo la Vingunguti katika Jiji la Dar es Salaam.*

Hali ya uhifadhi wa taka imeendelea kuwa si ya kuridhisha na hivyo kuchangia katika kuenea kwa taka katika maeneo mbalimbali. Idadi kubwa ya wakazi wamekuwa wakiendelea kutumia vyombo duni vya kuhifadhia taka kama vile mifuko ya viroba, ndoo zailizochakaa, mifuko ya plastiki nk. Hali hii imesababisha kuenea kwa taka katika maeneo mbalimbali na kusababisha athari mbalimbali za kiafya kwa jamii.



***Kielelezo Na. 2: Hali ya uhifadhi wa taka katika baadhi ya maeneo nchini.***

Aidha, hali ya usafirishaji wa taka nayo imekuwa si yakuridhisha katika maeneo mengi nchini. Vifaa vinavyotumika kusafirisha taka ikiwemo magari, trekta, na vyombo vingine vimekuwa katika hali mbaya na hivyo kuruhusu taka kumwagika wakati wa kusafirisha na hivyo kuendelea kuchangia katika uchafuzi wa mazingira



***Kielelezo Na. 3: Hali ya vyombo vya kusafirisha taka.***

Kukosekana kwa utaratibu wa utupaji wa taka umekuwa ni miongoni mwa changamoto za udhibiti wa taka nchini. Madampo mengi yakiwemo yale ya kisasa yamekuwa katika hali isiyoridhisha. Utaratibu wa utupaji na usimamizi wa taka kwenye madampo umekuwa ukichangia uchafuzi wa mazingira ikiwemo utiririshaji wa maji machafu (*leachate*) ambao ni hatari kwa afya za binadamu na ustawi wa mazingira.



***Kielelezo Na.4: Hali ya dampo la Chidaya katika jiji la Dodoma (Kushoto) na Muriet katika Jiji la Arusha (Kulia).***

*Kielelezo Na.5: Hali ya dampo la Pugu Kinyamwezi katika jiji la Dar es Salaam.*

## 2.2 Uzoefu wa udhibiti wa taka ngumu kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia tena Rejeleza kutoka nchi nyingine

Utekelezaji wa Mpango wa ***Punguza*, *Tumia Tena*, *Rejeleza*** kwa kiasi kikubwa unatofautiana katika ngazi mballimbali za uzalishaji taka. Hii inatokana na kutofautiana kwa aina ya taka zinazozalishwa, jinsi zinavyozalishwa na namna mfumo wa usimamizi katika eneo taka hizo zinazopozalishwa. Kwa muktadha huo sehemu hii itajikita katika kuelezea uzoefu wa kutekeleza dhana ya Punguza, Tumia Tena, Rejeleza katika Ngazi ya Kaya, Viwanda na Taasisi nyingine.

### 2.2.1 Uzoefu wa Utekelezaji wa Mpango wa Punguza, Tumia Tena, Rejeleza Katika Ngazi ya Kaya

#### *1.2.1.1 Uzoefu kutoka Mji Wa Hoi An, Vietnam*

Hoi An ni miongoni mwa miji katika nchi ya Vietnam yenye wakazi takriban 90,150 na kukadiriwa kuzalisha kiasi cha taka tani 80,925 kwa siku (Hoi An Natural Resources and Environmental Committee, 2011).

Katika kutekeleza Mkakati wa usimamizi na udhibiti wa Taka Ngumu Mji wa Hoi An unatekeleza Mpango wa *Punguza,Tumia Tena na Rejeleza*, kwa awamu 2. Awamu ya kwanza ilianza mwaka 2012 kwa majaribio katika Kata 4. Awamu ya 2 ilianza mwaka 2014 na kuhusisha Kata zote na kufanya mji wa Hoi An kuwa mji wa kwanza kutekeleza mpango wa *Punguza, Tumia Tena na Rejeleza* kwa mji mzima katika nchi Vietnam.

Mji wa Hoi An, ulitumia viongozi wa wakilishi wa Wananchi katika ngazi ya Kata kuwaelekeza wananchi kutenganisha Taka katika makundi matatu; Taka zinazooza, Taka zisizooza na Taka zinazopaswa kurejelezwa. Taka zinazooza zimewekewa utaratibu wa kukusanywa kila siku ya Jumatatu, Jumatano na Ijumaa. Taka zisizooza hukusanywa siku ya Jumanne, Alhamisi na Jumamosi. Taka za kurejelezwa wananchi wamekuwa wakiziuza moja kwa moja kwa warejelezaji au kuwapatia wakusanya taka za kurejeleza wasio rasmi (Waste pickers).

Aidha, kutokana na uhaba wa rasilimali fedha, maeneo ya vijijini na yale ya pembezoni mwa Mji walielekezwa kuzishughulikia taka zinazooza kwenye maeneo yao.

Ukusanyaji wa Taka katika Mji wa Hoi An, umekuwa ukifanywa katika ngazi kubwa 2. Ngazi ya kwanza ni katika Mitaa yenye barabara kubwa zinazopitika kwa urahisi ambayo hufanywa na Magari ya kusaga taka (Compactor Trucks) yanayomilikiwa na Manispaa. Magari haya hupita kwenye barabara kubwa na kukusanya taka zilizowekwa kwenye maeneo ya kukusanyia taka kando kando mwa barabara. Ngazi ya pili ni katika maeneo yenye barabara nyembamba zisizopitika kwa urahisi kwa kutumia magari makubwa ya Manispaa. Katika maeneo haya huduma ya kuzoa taka hufanywa na vikundi vya wanajamii kwa kutumia mikokoteni na kuzipeleka kwenye barabara kubwa ambapo

huchukuliwa na magari ya Manispaa. Taka zote zinazooza zilizokusanywa na Manispaa na vikundi vya kijamii hupelekwa kwenye mtambo wa kutengeneza mbolea. Taka zisizooza hupelekwa kuteketezwa katika dampo.

Tathmini ya utekelezaji mradi wa katika Mji wa Hoi An imebaini ufanisi katika kutekeleza dhana ya Punguza, Tumia Tena, Rejeleza unahitaji yafuatayo:

i. **Kuwepo kwa Mtambo wa utengenezaji Mbolea.** Asilimia 53.12 ya taka zinazozalishwa katika mji wa Hoi An ni taka zinazooza. Kuanzia mwaka 2012 Manispaa imekuwa na mpango wa kuhakikisha taka zinazooza zinapunguzwa kwa kutengeneza mbolea. Eneo lenye ukubwa wa Hekta 5.4 limetengwa kwa ajili ya kiwanda cha kutengeneza mbolea. Jumla ya tani 55 kwa siku hutengenezwa mbolea huku ajira 37 zikizalishwa katika mtambo huo.

ii. **Kuwepo wa soko la vifaa vinavyofaa kurejelezwa.** Katika Mji wa Hoi An, kuna jumla ya Maduka 17 yanayohusika na ununuzi wa Vifaa vinavyorejelezwa (Trinh, 2015). Maduka haya yananunua jumla ya tani 3 kila siku. Hii ni takribani asilimia 4.6 ya Taka zote zinazozalishwa katika Mji wa Hoi An.

iii. **Kuwepo kwa kanuni ya kulazimisha utenganishaji wa Taka.** Katika Mji wa Hoi An, kutotenganisha Taka ni kosa kwa mujibu wa sheria. Mtoa huduma ya uzoaji Taka akigundua taka zilizowasilishwa na mzalishaji hazijatenganishwa atamlazimisha mzalishaji wa taka hizo kurudi na taka zake nyumbani kama hatua ya awali. Aidha, kama mzalishaji huyo wa Taka ataamua kutorudi nazo nyumbani atalazimika kulipa faini ya fedha taslimu. Hii pia inaambatana na kuandikiwa

barua ya onyo kutoka manispaa na kupunguziwa baadhi ya fursa wanazopata jamii kutoka Manispaa.

#### *2.2.1.2 Uzoefu kutoka Mji wa Hanoi, Vietnam (2006- 2009)*

Mji wa Hanoi, Vietnam katika kipindi cha Mwaka 2006 -2009 ulianzisha Mradi wa kutekeleza dhana ya *Punguza, Tumia Tena na Rejeleza* (3R) katika Kata 4 kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Japan (JICA). Mpango huu ulilenga kujikita zaidi katika urejelezaji wa taka zinazooza. Kazi kubwa katika mradi huu ilikuwa ni kutoa elimu na mafunzo ya namna ya utekelezaji wa dhana ya *Punguza, Tumia Tena na Rejeleza*. Kwa kushirikiana na wadau elimu ilitolewa kwa kufanya vikao na wana jamii pamoja na kutembelea nyumba hadi nyumba kutoa elimu kwa Wananchi. Vilevile elimu ilitolewa kwa wanafunzi mashuleni mara mbili kwa wiki. Zaidi ya vipindi 300 vya redio vilifanyika katika kipindi cha mradi kuelimisha jamii kutekeleza dhana ya *Punguza, Tumia Tena na Rejeleza*. Mradi pia ulifanikiwa kuwahamasisha vijana wa kujitolea na vikundi vya kina mama kushiriki katika uhamasishaji na utekelezaji wa mradi.

Aidha, mradi pia ulihusisha upanuzi wa mtambo wa kutengeneza mbolea na kutekeleza mkakati wa kuongeza mahitaji ya mbolea. Tathmini ya utekelezaji wa mradi huu imebaini mambo yafuatayo:

i. Utekelezaji wa mpango wa Punguza, Tumia Tena, Rejeleza unahitaji Kuwepo kwa Mpango kazi madhubuti unaoonyesha namna ya kuzishughulikia taka zilizotenganishwa pamoja na kutenga bajeti ya kutosha kutekeleza kampeni ya kuhamasisha utekelezaji mpango.

ii. Kuweka mwongozo unaoainisha namna wananchi watakavyoshiriki katika utekelezaji wa Mpango. Hii inaweza kuhusisha namna ya kutenganisha taka, muda wa kuchukua taka na eneo/ maeneo ya kuchukulia taka.

iii. Kufanya kampeni za uhamasishaji pamoja na kusimamia sheria ipasavyo.Uzoefu wa Vietnam unaonyesha usimamiaji wa sheria, kanuni na taratibu kikamilifu unachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Mpango.

iv. Mamlaka zinazohusika na udhibiti wa taka kuhakikisha kabla ya kuanza kutekeleza mpango wa Punguza. Tumia Tena na Rejeleza elimu ya kutosha inatolewa kwa jamii ili kuongeza uelewa na utayari wa ushiriki wao.

v. Mamlaka inayohusika na udhibiti na usimamizi wa taka ngumu kuhakikisha huduma ya uhakika ya kuzishughulikia taka zilizotenganishwa inapatikana. Ushiriki wa wananchi unaweza kuwa mkubwa iwapo wataona jitihada zao za kutenganisha taka zina matokeo chanya. Kitendo cha kutenganisha taka na kutoshughulikiwa kunaweza kuathiri utekelezaji wa mpango.

#### *2.2.1.3 Uzoefu kutoka Nchi ya Japan*

Japani ni miongoni mwa Nchi zinazofanya vizuri katika kudhibiti taka ngumu kupitia mfumo wa PTR. Mafanikio ya Japan kwa kiwango kikubwa yamechangiwa na uwepo wa sheria wezeshi zilizochochea wadau mbalimbali kushiriki katika utekelezaji wa mfumo wa PTR (Srinivas, 2015). Miongoni mwa sheria hizo ni pamoja na;

- *Sheria ya Msingi ya kuanzisha mfumo mzunguko katika usimamizi wa Taka ya mwaka...(Fundamental Law for establishing a Sound Material Cycle Society)*

- *Sheria ya Usimamizi wa Taka na Usafi (Waste Management and Public Cleansing Law)*

- *Sheria ya kuhamasisha matumizi ya rasilimali zinazoweza kurejelezwa ya mwaka...(Law for the Promotion of Utilization of Recyclable Resources)*

- *Sheria ya vifungashio na vibebeo vinavyorejelezeka ya mwaka... (Container and Packaging Recycling Law)*

- *Sheria ya vifaa vya umeme majumbani vinavorejelezeka ya mwaka... (Electric Household Appliance Recycling Law)*

- *Sheria ya urejelezaji wa malighafi za Ujenzi ya mwaka... (Construction Material Recycling Law)*

- *Sheria ya urejelezaji wa vyakula ya mwaka... (Food Recycling Law)*

- *Sheria ya urejelezaji wa magari chakavu ya mwaka... (End-of-life Vehicle Recycling Law) na*

- *Sheria ya kuhamasisha Manunuzi yanayozingatia hifadhi ya Mazingira ya mwaka... (Law on Promoting Green Purchasing).*

Kwa mfano, kwa kupitia sheria ya kuhamasisha manunuzi yanayozingatia hifadhi ya Mazingira *(Law on Promoting Green Purchasing)* kila taasisi ya Serikali inalazimika kuwasilisha taarifa kila Mwaka kuonyesha namna walivyofanya manunuzi ya bidhaa na huduma kwa kuzingatia hifadhi ya Mazingira (*Green Purchase*)

Aidha, Pamoja na uwepo wa sheria mbalimbali mafanikio ya Japani katika utekelezaji wa Mfumo wa PTR pia yamechangiwa na uwekezaji walioufanya katika uelimishaji wa jamii, ubunifu wa teknolojia mbalimbali zinazowezesha na kuchochea utekelezaji wa mfumo wa PTR, ushirikiano wa karibu baina ya Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi na uwepo wa masoko kwa bidhaa zinazorejelezwa (Srinivas, 2015).

### *2.2.1.4 Uzoefu wa Utekelezaji wa Dhana ya Punguza, Tumia Tena, Rejeleza Viwandani*

Katika sehemu hii Kampuni ya Sweden inayojihusisha na uzalishaji wa nguo aina ya "Jeans" na kampuni za Samsung na Dell zinazojihusisha na uzalishaji wa vifaa vya umeme na vile vya kielektroniki zimetumika kama mifano bora katika utekelezaji wa dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza.

#### *a) Uzoefu kutoka Kampuni ya Kushona Nguo Ya Nudie Jeans-Nchini Sweden*

Sekta ya ushonaji wa nguo ni miongoni mwa sekta 10 zinazoongoza kwa uzalishaji wa taka nyingi duniani (Athanasios, 2018). Hii inatokana na mnyororo mkubwa wa thamani katika sekta hii ambao huanzia kwenye uzalishaji wa malighafi, usafirishaji na usimamizi wa malighafi, uchakataji wa malighafi katika viwanda, ushonaji wa nguo, usafirishaji wa nguo hizo, uuzaji wa rejareja, na hatimaye utupaji wa nguo zilizokwisha chakaa.

Kampuni ya *Nudie Jeans* imekuwa miongoni mwa makampuni yaliyojiwekea utaratibu wa kutekeleza dhana ya *Punguza, Tumia Tena, na Rejeleza* katika shughuli zake. Kampuni hii imeanzisha mfumo wa kutoa punguzo la asilimia 20 kwa mteja atakayerudisha nguo ya zamani aliyokwisha itumia katika maduka yao yaliyopo katika Majiji ya *London, Gothenburg* na

*Stockholm*. Nguo iliyorudishwa husafishwa na kuuzwa tena kama Mtumba (Nudie Jeans, 2014). Aidha kama ikitokea nguo iliyorudishwa ina hali mbaya kiasi cha kutoweza kuvalika tena, nguo hiyo hurejelezwa kiwandani. Vilevile Kampuni ya *Nudie Jeans* hutoa bure huduma ya kuzifanyia matengenezo nguo zilizoharibika kwa wateja wao.

b) Uzoefu kutoka Kampuni za kuzalisha vifaa vya umeme na elektroniki ya Samsung

Kampuni ya Samsung imeandaa na kuweka utaratibu wa kutoa hudumu ya kufanya matengenezo bure kwa vifaa vya wateja wao kwa lengo la kuhakikisha wateja wao wanatumia vifaa hivyo kwa muda mrefu na hivyo kupunguza uzalishaji wa Taka. Aidha, Kampuni hii imekuwa ikitoa udhamini (warranty) wa kati ya miaka 2 mpaka 10 kwa kifaa au sehemu muhimu ya kifaa ili kuhakikisha vifaa vyao vinatumika kwa muda mrefu kadiri iwezekanavyo. Vilevile kampuni hii imetenga maeneo mahsusi ya kufanyia matengenezo bidhaa za wateja wao bure pamoja na kuanzisha mfumo wa kielektroniki inayoweza kumuongoza mteja kujifanyia matengenezo madogo madogo mwenyewe.

Katika kuhakikisha bidhaa wanazozalisha zinarejelezeka kwa urahisi Kampuni ya Samsung kuanzia mwaka 2015 ilijiwekea lengo la kuhakikisha asilimia 30 ya kompyuta za mezani wanazozalisha zinatengenezwa kwa plastiki ambayo inaweza kurejelezwa kwa urahisi. Lengo hili pia lilihusisha utengenezaji wa *charger* na *earphone* za simu za mkononi na baadhi ya vifaa vya ndani vya simu hizo.

### *2.2.1.5 Uzoefu wa Utekelezaji wa Dhana ya Punguza, Tumia Tena, Rejeleza Sehemu za Maofisi*

Katika kutekeleza dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza katika sehemu za Ofisi, Kampuni ya PwC ya nchini Sweden ilfanya yafuatayo:

i. **Kuhamasisha mabadiliko ya tabia kwa watumishi wake:** Miongoni kwa kampeni zilizoanzishwa na kampuni hii ni ile ya "Tuongee Uchafu" (Let's talk rubbish) iliyoanza kutekelezwa mwaka 2016. Kampeni hii ililenga katika kuwezesha watumishi wake kushiriki kwenye upunguzaji wa taka kwa kufikisha ujumbe kwa namna ya mzaha na utani kupitia vikatuni na jumbe mbalimbali hasa baada ya chakula cha mchana kwenye baruapepe kuwakumbusha kuzitenganisha taka baada ya kupata chakula cha mchana. Kampeni hii ilipokolewa vizuri na watumishi na kupelekea kampuni ya PwC kuvunja rekodi yake ya utenganishaji taka kwa mwaka huo

ii. **Kutengeneza bidhaa zilizoharibika ili zitumike tena:** Kampuni ya PwC imeingia kwenye mashirikiano na kampuni ya Tier 1 na S2S kwa ajili ya kuzitengeneza simu za mkononi na kompyuta mpakato na kuziuza tena. Mpango huu umesaidia kuongeza kipato na pia kupunguza kiasi cha taka zilizopaswa kupelekwa dampo.

iii. **Kutengeza mbolea au nishati kutokana na taka za mabaki ya vyakula.** Kampuni ya PwC inashirikiana na kampuni ya Uptown Oil kuzalisha nishati inayotumika kama chanzo cha joto kutokana na mafuta yalitumika katika migahawa iliyopo kwenye ofisi zake. Nishati

inayozalishwa imetumika katika mifumo ya viyoyozi hasa nyakati za joto na mifumo ya kuongeza joto katika nyakati za baridi na mifumo ya umeme kwenye majengo yao. Hii imesaidia kupunguza gharama za nishati pamoja na kiwango cha taka kinachopelekwa dampo.


iv. **Kurejeleza karatasi zilizotumika:** Kampuni PwC imeingia makubaliano na Kampuni ya Kijerumani ya Steinbeis inayojihusisha na utengenezaji wa karatasi kwa ajili ya kurejeleza karatasi zilizokwisha kutumika. Kampuni ya PwC huzinunua tena karatasi hizo baada ya kurejelezwa. Kwa wastani PwC hurejeleza karatasi walizotumia kwa takribani mara 20.

v. **Kurejeleza Sare za Kazini.** Kampuni ya PwC imeanzisha mfumo wa kuhakikisha mtumishi anarudisha sare ya zamani kabla hajapatiwa sare mpya. Kampuni hii imeingia katika mashirikiano na kampuni ya JMP Wilcox, wataalamu wa kurejeleza nguo ambao hubadilisha nguo zinazorejelezwa kuwa bidhaa nyingine.

## 2.3 Mfumo wa Dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza

### 2.3.1 Tafsiri ya Mfumo wa Punguza, Tumia Tena na Rejeleza katika Usimamizi wa Taka Ngumu

Dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza inamaanisha kupunguza kiasi cha taka kinachozalishwa katika maeneo mbalimbali katika shughuli za kila siku na hatimaye kupunguza kiasi cha taka kinachosafirishwa kwenda dampo.




*Kielelezo Na. 6: Mfumo wa Punguza, Tumia tena na Rejeleza katika Usimamizi na Udhibiti wa Taka ngumu.*

### a) Punguza

Mbinu hii inahusisha kupunguza uzalishaji wa Taka. Miongoni mwa mifano ya kupunguza uzalishaji wa taka ni kama vile:

i. Kupunguza manunuzi ya vitu visivyo vya lazima, kununua bidhaa kwa pamoja na kutumia vibebeo vinavyohifadhi bidhaa nyingi kwa wakati mmoja kama vile vikapu. Hali hii inasaidia kupunguza idadi ya vifungashio ambavyo vinaongeza uzalishaji wa Taka.

ii. Ununuaji na utumiaji wa bidhaa zinazodumu kwa muda mrefu pia ni sehemu ya utekelezaji wa mbinu ya kupunguza uzalishaji wa taka.

iii. Kupunguza matumizi ya karatasi kwa kutumia mifumo ya kielektroniki kama vile barua pepe na kanzidata.

iv. Kuepuka kununua vibebeo vya vyakula pale unaponunua vyakula vya pakiti ambavyo vinaweza kushikwa mkononi.

v. Matumizi ya vibebeo vinavyobeba bidhaa nyingi kwa pamoja



***Kielelezo Na. 7: Mfano wa kibebeo cha bidhaa nyingi kwa pamoja.***

**b) Tumia tena**

Mbinu hii inahusisha utumiaji wa taka kwa matumizi mengine tofauti na matumizi ya awali yaliyokusudiwa. Mifano ya utekelezaji wa Mbinu hii ni kama vile:

i. Vyakula vilivyobaki vinaweza kutumika kulishia mifugo



***Kielelezo Na. 8: Mabaki ya vyakula yakitumika kama chakula cha mifugo.***

ii. Mabaki ya vitu vinavyooza vyaweza kutumika kutengenezea mbolea kwa ajili ya kilimo, cha msingi ni kuhakikisha afya ya binadamu inazingatiwa katika matumizi hayo.

iii. Ndoo za rangi baada ya kuisha rangi kutumika kama vyombo vya kuoteshea na kutunza maua.

iv. Matumizi ya vitambaa badala ya “tissues” au matumizi ya kalamu zinazoweza kujazwa wino (ink refilled pen) au Matumizi ya betri zinazoweza kuchajiwa.

v. Samani chakavu (viti, meza, makabati) kukarabatiwa na kutumika tena.



Kabla Baada

***Kielelezo Na. 9: Makabati yaliyokarabitiwa na kutumika tena.***

vi. Matumizi ya vyombo vinavyoweza kuoshwa na kutumika tena badala ya kutumia vyombo visivyoosheka "disposables"

vii. Kutumia Majagi na vikombe badala ya chupa za maji kwenye vikao mbalimbali

**c) Rejeleza**

Mbinu hii inahusisha utumiaji wa taka kama malighafi ya kuzalisha bidhaa nyingine.

i. Chupa za plastiki zinaweza kutumika kama malighafi kutengeneza bidhaa nyingine za plastiki kama vile mazulia, mapazia, kamba na chupa.



***Kielelezo Na. 10: Chupa za plastiki zimerejelezwa na kutengenezwa fulana.***

ii. Matairi ya magari yanaweza kuengenezwa samani



*Kielelezo Na. 11: Matairi chakavu yanaweza kutengenezwa samani.*

iii. Taka zinazooza zinaweza kutengenezwa mkaa jadidifu.



*Kielelezo Na. 12: Taka zonazooza zinaweza kutengenezwa mkaa jadidifu.*

### 2.3.2 Faida ya Mwongozo

a) Kupunguza kiasi cha taka kinachozalishwa na kusafirishwa kwenda dampo.

b) Kuongezeka upatikanaji wa malighafi viwandani na hivyo kupunguza matumizi ya rasilimali ghafi.

c) Upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kurejeleza taka.

d) Kuongeza upatikanaji wa mbolea (Mboji).

e) Kuongeza muda wa matumizi ya madampo ya kisasa.

f) Kuongezeka kwa fursa za ajira na kodi zitokanazo na viwanda vya urejelezaji wa taka.

### 2.3.3 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kutumiwa na wadau mbalimbali ikiwemo: Wazalishaji wa taka ngumu zikiwemo Kaya; Maeneo ya biashara; Vyombo vya usafiri wa nchi kavu; Taasisi zikiwemo Wizara, Idara za Serikali na Sekta binafsi; Viwanda; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi za Elimu; Watoa huduma za uzoaji wa taka ngumu; na Warejelezaji wa taka.

# SURA YA TATU

## 3.0 MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MFUMO WA PUNGUZA, TUMIA TENA NA REJELEZA (PTR)

### 3.1 Lengo la Mwongozo

Lengo la Mwongozo huu ni kuweka mfumo unaowezesha kupunguza uzalishaji wa taka, kuhamasisha matumizi mbadala ya taka na kuongeza kasi ya urejelezaji wa taka nchini kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza.

### 3.2 Madhumuni ya Mwongozo

Mwongozo huu unatoa maelekezo mahsusi ya namna ya kutekeleza dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza kwa makundi mahususi yanayohusisha uzalishaji mkubwa wa taka ngumu. Uzalishaji huu mkubwa wa taka ngumu unahusisha maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo ya Makazi ngazi ya kaya, Maeneo ya biashara kubwa na ndogo hususan masoko, maduka makubwa na madogo, maghala ya kuhifadhi bidhaa mbalimbali, karakana, migahawa, hoteli vituo vya usafiri na nyumba za kulala wageni. Aidha, maeneo mengine ni pamoja na taasisi za Serikali na binafsi. Taasisi za elimu zikiwemo Shule za awali, msingi sekondari; vyuo vya kati na juu, viwanda shughuli za ujenzi na sehemu za huduma za afya.

### 3.3 Maeneo ya utekelezaji wa Mwongozo

Maeneo yatakayohusika na utekelezaji wa Mwongozo huu ni pamoja na makazi, biashara, viwanda, taasisi mbalimbali kama vile wizara na idara za serikali, taasisi za elimu, viwanda, sekta

ya ujenzi, maeneo ya huduma za afya na watoa huduma za ukusanyaji wa taka.

### 3.1.1 Maeneo ya makazi ngazi ya Kaya

Taka ngumu zinazozalishwa katika ngazi ya kaya hujumuisha taka mbalimbali zikiwemo taka zinazooza zikihusisha mabaki ya chakula, taka za jikoni, majani na matawi ya miti, nyasi za bustani, mbao, karatasi, maboksi, plastiki, Vyuma chakavu, kioo, taka zitokanazo na vifaa vya umeme na elektroniki, na zile zitokanazo na shughuli za ujenzi. Aidha, katika kuhakikisha tunalinda mazingira yetu, afya ya binadamu na kupunguza gharama za udhibiti na usimamizi wa taka ngumu ni muhimu kutumia mbinu mbalimbali ambazo ni pamoja na kutumia dhana ya punguza uzalishaji wa taka, tumia tena na rejeleza taka kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

#### a) Punguza

Hatua zifuatazo zinaweza kuchukuliwa katika ngazi ya kaya kwa lengo la kupunguza kiasi cha ujazo wa taka ngumu zinazozalishwa.

i. Kununua bidhaa kwa kiasi kinachohitajika tu.

ii. Kununua bidhaa kwa jumla ili kupunguza kiasi cha vifungashio ambavyo baadaye huishia kuwa taka.

iii. Kutumia vibebeo maalumu vya kudumu kama vile vikapu kwa ajili ya kubebea bidhaa.

iv. Kununua bidhaa ambazo zinadumu kwa muda mrefu ili kupunguza manunuzi ya mara kwa mara.

v. Kuchambua na kuuza au kugawa vitu ambavyo havihitajiki kama vile vyakula, nguo, makopo na vinginevyo kwa watu wengine wenye uhitaji.

vi. Kuhifadhi vitu vile ambavyo vinaweza kutumika baadaye ili visiharibike na kuwa taka mfano vyakula (ndizi, mihogo, viazi) vinavyokaushwa kwa kutumia jua ili viweze kutumika badaye.

Kwa kufuata hatua hizi tunaweza kupunguza kiasi kikubwa cha taka ngumu zinazozalishwa kwenye ngazi ya kaya.

### b) Tumia Tena

Katika kuhakikisha kuwa taka ngumu zinatumika tena ni muhimu kukuza uelewa wa kutambua thamani ya taka ulizonazo na kuzipa matumizi mbadala ambayo yataleta faida kwa jamii. Ili kutekeleza dhana ya Tumia Tena wahusika katika ngazi ya kaya wanapaswa kuzingatia masuala yafuatayo: -

i. Kutumia mabaki ya bidhaa zinazooza kutengenezea mbolea kwa ajili ya kilimo, bustani na maua

ii. Kutumia mabaki ya vyakula kulishia mifugo kama vile paka, mbwa na kuku

iii. Kutumia ndoo, makopo na chupa zilizokwishatumika kupandia maua na urembo

iv. Nguo ambazo hazitumiki tena kama mavazi zaweza kupewa matumizi mengine kama kugawa kwa wahitaji, kudekia, kutengenezea makochi au sehemu yeyote inayofaa kuzitumia

### c) Rejeleza

Katika kutekeleza dhana ya Rejeleza, baadhi ya taka zinazozalishwa majumbani hususan plastiki, kioo, chuma chakavu, taka za vifaa vya umeme na elektroniki zinaweza kurejelezwa na kuwa malighafi ya viwandani, masuala yafuatayo

wanapaswa kuzingatia:-

i. Chambua, tenganisha na hifadhi taka zenye asili ya chuma ili kupata malighafi ya kutengenezea bidhaa nyingine. Taka hizo zinaweza kuuzwa kwa wenye viwanda vya urejelezaji na kuwa chanzo cha mapato

ii. Chambua, tenganisha na hifadhi taka zitokanazo na vifaa vya kielektroniki na umeme kama vile Kompyuta mbovu, simu mbovu, betri na vifaa vya umeme vya majumbani. Taka hizi zinaweza kuuzwa kwa wafanya biashara wa viwanda vidogo na mafundi wenye uhitaji wa vifaa hivyo

iii. Chambua, tenganisha na hifadhi taka zenye asili ya plastiki, kioo na kuziuza kwa wenye viwanda vya urejelezaji wa vifaa hivyo ili vitengeneze bidhaa nyingine za plastiki, kioo au kuwa malighafi ya kutengeneza bidhaa nyinginezo

### 3.1.2 Maeneo ya biashara

Taka zinazozalishwa katika maeneo ya biashara kama vile Masoko, maduka makubwa na madogo, maghala, Karakana, Kantini, Migahawa, Hoteli na nyumba za kulala wageni ni pamoja na: taka zitokanazo na vifaa vya plastiki, vifaa vya umeme na elektroniki, Vyuma chakavu, Chupa (kioo), na Taka zinazooza kama vile mabaki ya chakula, mbao na karatasi.

Katika kutekeleza dhana ya PTR katika maeneo ya biashara ni muhimu kuzingatia masuala yafuatayo:-

**a) Punguza**

i. Kufungasha bidhaa mbalimbali kwa kutumia vifungashio

vichache ili kupunguza uzalishaji wa taka katika maeneo ya biashara

ii. Kununua na kuuza bidhaa za kieletroniki na umeme zenye ubora ili kupunguza ongezeko la uzalishaji wa taka zitokanazo na vifaa hivi

iii. Kuepuka kununua vifaa chakavu vya umeme na kielektoniki ili kupunguza ongezeko la uzalishaji wa taka zitokanazo na vifaa hivi

iv. Kununua bidhaa za kioo zenye ubora na ujazo mkubwa zinazoweza kutumika zaidi ya mara moja katika shughuli za mahoteli, migahawa nyumba za kulala wageni ili kupunguza uzalishaji wa Taka unaoweza kutokana na bidhaa hizo

v. Kuchapisha nyaraka pande zote mbili za karatasi badala ya upande mmoja ili kupunguza uzalishaji wa taka

**b) Tumia tena**

i. Kutumia taka ngumu zinazooza kutoka kwenye masoko, migahawa, mahoteli, maduka makubwa kama vile mabaki ya chakula kama chakula cha mifugo

ii. Kutumia vyombo vya plastiki vinavyoweza kutumika zaidi ya mara moja mfano mitungi ya kuhifadhi maji ili kupunguza uzalishaji wa taka utokanao na chupa za plastiki

iii. Migahawa, kantini na hoteli, kutumia vyombo vinavyoweza kutumika zaidi ya mara moja kuhifadhia vyakula badala ya magezeti, au *aluminium foils*

iv. Kuchambua, kutenganisha na kukarabati vifaa umeme na kielektroniki vyenye hitilafu ndogo ili vitumike tena

v. Kutumia maboksi yatokanayo na vifungashio kwa matumizi mengine

vi. Matairi chakavu yatumike kwa ajili ya kuzalisha nishati na kukarabati (retread) matairi hayo ili yaweze kutumika tena kwa lengo la kupunguza taka

**c) Rejeleza**

i. Mabaki ya vitu vinavyooza kama vile mabaki ya vyakula, matunda, vifungashio vitokanavyo na mazao ya kilimo yarejelezwe ili kutengeza mboji kwa matumizi ya shughuli za kilimo

ii. Taka zenye asili ya chuma kama vile chuma chakavu zikusanywe, zihifadhiwe na ziuzwe kwa mujibu wa Kanuni ya Udhibiti wa Taka hatarishi

iii. Taka zitokanazo na bidhaa za plastiki kama vile chupa za plastiki zikusanywe, zihifadhiwe na kupelekwa kwenye viwanda vya kurejeleza

iv. Taka zitokanazo na vifaa vya umeme na kielektroniki ikiwa ni pamoja na betri chakavu zikusanywe, zihifadhiwe na kusafirishwa kwa mujibu wa Kanuni ya Udhibiti wa Taka hatarishi

v. Taka zinazotokana na mabaki ya vyakula yanayozalishwa katika maeneo ya biashara, zitumike kuzalisha mbolea itakayotumika kwenye bustani au kuuzwa kwa wafanyabishara wanaozalisha mboji

### 3.1.3 Taasisi

Taasisi zinazohusishwa ni Wizara, Wakala na Idara za Serikali pamoja na Taasisi Binafsi. Katika utekelezaji wa majukumu

yao ya kila siku taasisi hizi pia huzalisha taka ikiwa ni pamoja na taka ngumu. Taka zinazozalishwa kwa kiasi kikubwa ni zile zitokanazo na karatasi, vifungashio, vibebeo, mabaki ya chakula na vyombo vya kulia chakula, chupa za plastiki, vifaa vya umeme na elektroniki. Kwa kutumia mwongozo huu Taasisi zitafaidika kwa kupunguza gharama za ununuzi wa bidhaa na gharama za ukusanyaji na utupaji taka na hivyo kuchangia katika hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu. Katika kutekeleza dhana ya PTR katika Taasisi masuala yafuatayo yazingatiwe: -

**a) Punguza**

i. Kuhakiki kwa makini na kuchapisha nyaraka pande mbili ili kupunguza taka zinazotokana na karatasi

ii. Kutunza nyaraka mbalimbali kwenye mitandao na kanzidata

iii. Kuandaa na kusambaza taarifa mbalimbali kwa njia ya barua pepe

iv. Kutumia vitambaa vinavyoweza kutumika zaidi ya mara moja katika kufanya usafi

v. Kuepuka matumizi ya bidhaa zinazotumika mara moja tu na kutupwa kama vile sahani vikombe, vijiko na mirija ya plastiki

vi. Kutumia chupa kubwa za maji ya kunywa badala ya kununua chupa ndogo ndogo ili kupunguza taka za plastiki

vii. Kurudisha vifungashio kama vile makasha, maboksi na makopo kwa wazalishaji au wasambazaji wa bidhaa

viii. Kama kuna ulazima wa taarifa fupi “memos” zilizochapishwa zipitishwe kwa kila mfanyakazi au ziwekwe kwenye mbao za matangazo

ix. Katika mikutano nyaraka za rejea zisichapishwe ila ziwasilishwe kwa wahusika kabla ya mkutano kwa barua pepe na wakati wa mkutano zioneshwe kielektroniki.

x. Ikiwa ni lazima kuchapisha nyaraka, zichapishwe nakala chache zitakazotumika kwa kushirikiana

xi. Kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa kutuma nyaraka kwa watumishi

xii. Kutumia vyombo vya kunywea chai/maji vinavyoweza kutumika zaidi ya mara moja ili kupunguza matumizi ya vyombo vinavyotumika mara moja kama chupa za plastiki haswa katika mikutano ya ndani

xiii. Kununua bidhaa zenye ubora na zinazodumu kwa muda mrefu

**b) Tumia tena**

i. Kama kuna bidhaa ambazo hazihitajiki ofisini kwako lakini bado zinaweza kutumika zitoe kwa watu au taasisi nyingine ili ziendelee kutumika. Bidhaa hizo ni kama vile maboksi ya vifungashio, betri za kuchaji, mashine za kubania karatasi

ii. Tumia tena karatasi zilizokwisha kutumika upande mmoja kuchapisha rasimu za taarifa na nyaraka

iii. Kutumia ndoo na makopo ya plastiki yaliyokwisha kutumika kwa ajili ya kupanda maua

iv. Kusanya mabaki ya chakula ili yatumike kama chakula cha mifugo

**c) Rejeleza**

i. Kusanya, tenganisha, hifadhi vizuri na peleka taka zinazorejelezwa kama vile karatasi na chupa za plastiki katika viwanda vya kurejeleza

ii. Tumia karatasi zilizotumika kama malighafi kwa ajili ya kutengenezea bidhaa nyingine kama vile bahasha, vinyago, mbao za matangazo na mkaa mbadala

iii. Kusanya, tenganisha, hifadhi vizuri taka zinazooza na kutengenezea mboji na mbolea zitakazotumika katika bustani

### 3.1.4 Taasisi za elimu

Maeneo ya taasisi za elimu kama vile shule za awali, msingi, sekondari na vyuo ni mojawapo ya wazalishaji wa taka ngumu. Taka zinazozalishwa katika maeneo haya kwa kiasi kikubwa ni karatasi, taka zinazooza na taka za plastiki, taka zitokanazo na vifaa vya umeme na kielektroniki. Katika kutekeleza dhana ya PTR katika Taasisi za elimu masuala yafuatayo yazingatiwe: -

a) Punguza

i. Tumia zaidi vifaa vya kielektroniki kwa ajili ya kufundishia badala ya kuchapisha kwenye karatasi ili kupunguza uzalishaji wa taka

ii. Hakiki kwa makini na chapisha nyaraka pande mbili ili kupunguza taka zinazotokana na karatasi

iii. Tunza nyaraka mbalimbali kwenye mitandao na kanzidata ili kupunguza kuchapa

iv. Andaa na sambaza taarifa mbalimbali kwa njia ya barua pepe

v. Kununua vifaa vya umeme na kielektroniki vyenye ubora ili kupunguza ongezeko la uzalishaji wa taka zitokanazo na vifaa hivi

vi. Tumia vyombo vyenye ubora kwa ajili ya kuhifadhi vyakula ili kupunguza taka

**b) Tumia tena**

i. Chambua, tenganisha na karabati vifaa vya umeme na kielektroniki vyenye hitilafu kidogo ili vitumike tena

ii. Kutumia tena karatasi zilizokwisha kutumika upande mmoja

iii. Kutumia mabaki ya chakula kama chakula cha mifugo

iv. Kutumia ndoo na makopo ya plastiki yaliyokwisha kwa ajili ya kupanda maua katika meneo ya shule na vyuo

**c) Rejeleza**

i. Kutumia karatasi zilizotumika kama malighafi kwa ajili ya kutengenezea bidhaa nyingine mfano; mkaa, vinyago na mbao za matangazo

ii. Kutumia mabaki ya Taka za chakula, majani na matawi ya miti kwa ajili ya kutengenezea mboji

iii. Kukusanya taka za plastiki na kuzipeleka katika viwanda vya kurejeleza ili kutengeneza bidhaa nyingine

iv. Tumia karatasi, maboksi kwa ajili ya kutengezea vibebeo

### 1.1.5 Viwanda

Kwa muktadha wa mwongozo huu, viwanda ni maeneo maalum yanayochakata malighafi kutengeneza bidhaa nyingine kama vile Viwanda vya nguo, Vinywaji, Chakula, Vifaa vya ujenzi, Karatasi, Mbao, Madawa na Vifungashio. Taka zinazozalishwa katika maeneo hayo ni pamoja na: Taka za Plastiki, Vyuma chakavu, Chupa za kioo, taka zinazooza, mbao, karatasi, Vifaa vya umeme na electroniki, pamoja na taka za kemikali na vifungashio vyake. Aidha, taka za kemikali na vifungashio vyake zikusanywe, zihifadhiwe na kusafirishwa kwa mujibu wa Kanuni ya Udhibiti wa Taka hatarishi.

Katika kutekeleza dhana ya PTR katika maeneo ya Viwanda masuala yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:-

**a) Kupunguza**

i. Kutumia teknolojia za uzalishaji bora viwandani kwa lengo la kupunguza uzalishaji taka

ii. Kununua na kutumia malighafi zenye ubora ili kupunguza uzalishaji wa taka

iii. Kutumia malighafi zenye kiwango kidogo cha viambata sumu ili kupunguza uzalishaji wa taka sumu

iv. Kununua malighafi kwenye vifungashio vichache

v. Kuzalisha bidhaa zenye ubora ambazo hazitaharibika kwa haraka ili kupunguza manunuzi ya mara kwa mara

**b) Tumia tena**

i. Kutumia vifungashio vya malighafi kwa matumizi mengine au kama malighafi ya viwanda vingine

ii. Kuchambua, kutenganisha na Kufanya marekebisho ya

baadhi ya vifaa mfano vifaa umeme na kielektroniki vyenye hitilafu kidogo ili viweze kutumika tena na kupunguza uzalishaji wa taka

**c) Rejeleza**

i. Kuchambua, kutenganisha na kuhifadhi taka zinazoweza kurejelezwa kwa kuziwekwa katika sehemu tofauti na taka ambazo haziwezi kurejelezwa

ii. Kuchambua na kutenganisha bidhaa ambazo hazikufikia kiwango cha ubora ili zitumike kama malighafi katika kiwanda husika au kiwanda kingine

iii. Kutumia taka za viwandani kuzalisha nishati mfano viwanda vya kuchakata mkonge

### 3.1.6 Sekta ya ujenzi

Shughuli za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa makazi huambatana na uzalishaji wa taka mbalimbali ikiwemo taka ngumu. Hivyo, katika kuhakikisha shughuli za ujenzi haziathiri mazingira ni muhimu kuhamasisha matumizi ya dhana ya punguza, tumia tena na rejeleza taka ngumu. Katika kutekeleza dhana hii masuala yafuatayo yazingatiwe ili kuleta ufanisi katika shughuli za usimamizi na udhibiti wa taka.

**a) Punguza**

i. Nunua vifaa vya ujenzi kulingana na mahitaji halisi ili kupunguza uzalishaji wa taka utokanao za sekta ya ujenzi (mfano rangi, mbao, saruji n.k)

ii. Fanya ununuzi wa pamoja wa vifaa vya ujenzi ili kupunguza vifungashio ambavyo baadaye huishia kuwa taka ngumu.

iii. Azima au kodi baadhi ya vifaa badala ya kuvinunua, mfano mbao za kufungia zege

**b) Tumia tena**

i. Tumia mabaki ya kokoto kama chanzo cha mchanga kwenye shughuli za ujenzi ili kupunguza utupaji holela wa mabaki hayo kwenye mazingira

ii. Tumia mabaki ya matofali kutoka kwenye majengo yanayobomolewa kwa ajili ya vifusi

**c) Rejeleza**

i. Tumia mabaki ya mbao kama nishati

ii. Rejeleza taka za ujenzi zinazooza kutengeneza mboji au chakula cha kuku

iii. Chambua, hifadhi na tenganisha taka zinazorejelezeka na kuzihifadhi na baadaye kuzipeleka kwenye viwanda vya urejelezaji

iv. Kutumia taka ngumu zitokanazo na shughuli za ujenzi kutengeneza tofali na kuzitumia kwenye shughuli za ujenzi

### 3.1.7 Huduma za afya

Taka zitokanazo na huduma za afya zinahusisha taka zinazozalishwa katika hospitali, Vituo vya afya, zahanati, vituo vya utafiti wa afya, maabara za huduma za afya ya binadamu na mifugo. Baadhi ya taka ngumu zinazozalishwa kutokana na huduma za afya ni pamoja na chupa na makopo ya dawa na kemikali, chupa na makopo ya sampuli, sindano na mirija ya maji na damu na vifungashio. Aidha, katika kutekeleza dhana ya

PTR watoa huduma za afya wazingatie yafuatayo;

**a) Punguza**

i. Kadiri inavyowezekana nunua vifaa tiba vya matibabu vinavyoweza kutumika tena ili kupunguza taka zitokanazo na bidhaa zinazotumika mara moja

ii. Nunua kiasi kidogo cha kemikali na dawa kulingana na mahitaji ili kupunguza uwezekano wa dawa kuharibika na kuwa taka

iii. Nunua kemikali za hospitali kwa pamoja ili kupunguza kiasi cha taka zitokanazo na vifungashio vya kemikali

iv. Kagua tarehe ya kuisha kwa dawa na usiruhusu dawa ambazo muda wa matumizi uliobaki ni mfupi na unapotumia dawa, anza kutumia dawa za zamani

v. Katika manunuzi ya bidhaa tumia watoa huduma wanaoweza kuleta bidhaa kidogo kidogo kwa haraka na wanaokubali kurudisha bidhaa ambazo hazijafunguliwa na wanaotoa huduma ya kukusanya taka zitokanazo na bidhaa zao

vi. Tumia vifaa vichache vya usafi katika kutoa huduma za usafi ili kupunguza uzalishaji wa taka

**b) Rejeleza**

Shughuli za huduma za afya huambatana na uzalishwaji wa taka hatarishi na taka zisizo hatarishi ambapo baadhi ya taka hizo zinaweza kurejelezwa kama vile karatasi, vifungashio na maboksi. Aidha, Taka hatarishi pia zinaweza kutumika kuzalisha nishati kwa matumizi mengine iwapo zinatibiwa ili kuondoa vimelea vya magonjwa.

i. Kusanya, tenganisha, takasa na hifadhi vizuri vifungashio vya bidhaa za matibabu na peleka kwa wanaorejeleza

ii. Kuchoma au kuteketeza (Incinerate) taka za hospitali ili kuzalisha nishati

iii. Kusanya, tenganisha, safisha na hifadhi chupa zilizokuwa na bidhaa hatarishi na peleka kwenye viwanda vyenye uwezo wa kurejeleza chupa hizo

iv. Tenganisha mabaki ya chakula na taka nyingine za hospitali ili yatumike kwa ajili ya kutengenezea mboji

# SURA YA NNE

## 4.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Katika kuwezesha utekelezaji wa dhana ya PTR katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo ya Makazi ngazi ya kaya, Maeneo ya biashara kubwa na ndogo hususan masoko, maduka makubwa na madogo, maghala ya kuhifadhi bidhaa mbalimbali, karakana, migahawa, hoteli vituo vya usafiri, nyumba za kulala wageni na Taasisi zitakuwa na majukumu yafuatayo;

**a) Maeneo ya Makazi ngazi ya kaya**

i. Kuweka vyombo vitatu vya kutenganisha taka na kuhakikisha vimewekewa alama kulingana na makundi matatu ya taka zinazozalishwa (taka zinazooza, taka za plastiki na taka nyinginezo)

**b) Maeneo ya biashara**

i. Kuhamasisha wateja kubadili tabia na mitazamo kuhusu udhibiti wa taka ngumu na uhamasishaji wa dhana ya PTR

ii. Kuweka vyombo vitatu vya kutenganisha na kukusanyia taka vyenye mifuniko vikiwa na alama ya kutenganisha taka zinazooza, zisizooza na hatarishi

iii. Kuwa na makubaliano na wazabuni yanayolenga kupunguza vifungashio visivyo vya lazima, kutumika tena au vile vinavyoweza kurejelezwa

iv. Kuainisha fursa mbalimbali zilizopo katika utekelezaji wa dhana ya PTR

**c) Taasisi**

i. Kuhakikisha kuwepo vyombo vitatu vya kutenganisha taka (taka zinazooza, taka zisizooza na taka hatarishi)

ii. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa ajili ya kubadili tabia na mitazamo kuhusu udhibiti wa taka ngumu na uhamasishaji wa dhana ya PTR

iii. Kuweka tangazo karibu na mashine ya kuchapisha ikielekeza uchapishaji ufanyike kwa kazi zenye ulazima tu

iv. Kuhamasisha utenganishaji wa taka ngumu katika chanzo kuwezesha utekelezaji wa dhana ya PTR

v. Kutenga eneo la kukusanyia Taka ngumu zinazoweza kurejelezwa katika Taasisi

vi. Kuingiza vipengele vinavyohusu utekelezaji wa PTR kwenye mikataba yote wanayoingia

**d) Taasisi za elimu**

i. Kutoa mafunzo kwa wanafunzi/wanavyuo/wafanyakazi kwa ajili ya kuwajengea utamadani na mitazamo kuhusu udhibiti wa taka ngumu na uhamasishaji wa utekelezaji wa dhana ya PTR

ii. Kuweka vyombo vitatu vya kutenganisha taka (taka zinazooza, zisizooza na hatarishi) katika maeneo mbalimbali yaliyopo kwenye Taasisi husika

iii. Kuteua msimamizi atakayeratibu utekelezaji wa dhana ya PTR

iv. Kuunda au kutumia klabu za wanafunzi/wanavyuo ili kuhamasisha utekelezaji wa PTR

v. Kushindanisha na kutoa motisha kwa wanafunzi katika utekelezaji wa mpango wa PTR.

vi. Kuainisha wadau ambao wanaweza kushirikiana nao katika kutekeleza PTR

vii. Taasisi za elimu kuhakikisha taka zinazozalishwa katika maeneo yao zinapunguzwa, zinatumika tena kwa shughuli nyingine au zinarejelezwa kwa ajili ya matumizi mengine

**e) Viwanda**

i. Kuhakikisha kuwepo vyombo vitatu vya kutenganisha taka (taka zinazooza, taka zisizooza na taka hatarishi)

ii. Kuhamasisha utenganishaji wa taka ngumu katika chanzo kuwezesha utekelezaji wa dhana ya PTR

iii. Kutenga eneo la kukusanyia Taka ngumu zinazoweza kurejelezwa katika kiwanda

iv. Kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali zitakazowezesha utekelezaji wa Mwongozo

v. Kuingiza vipengele vinavyohusu utekelezaji wa PTR kwenye mikataba yote wanayoingia

vi. Kuweka miundombinu ya kukusanya na kutenganisha taka zitokanazo bidhaa zinazalishwa na kiwanda husika katika maeneo maalumu

vii. Kuhakikisha taka zinazotokana na mchakato wa urejelezaji kwa kiasi kikubwa zinatumika tena kama malighafi

viii. Kuandaa taarifa za urejelezaji ikiainisha kiasi na aina ya taka ngumu zinazorejelezwa

ix. Kuhakikisha matumizi ya teknolojia sahihi kwa lengo la kupunguza kiasi cha taka kinachozalishwa

x. Kutenga eneo la kukusanyia Taka ngumu zinazoweza kurejelezwa katika kiwanda

xi. Kuhakikisha kuwepo vyombo vitatu vya kutenganisha taka (taka zinazooza, taka zisizooza na taka hatarishi)

**f) Watoa huduma za afya**

i. Kuweka vyombo vyenye alama maalumu kwa ajili ya kutenganisha taka hatarishi na taka za kawaida zinazozalishwa

ii. Kutenga eneo maalumu kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu zinazoweza kurejelezwa au kutumika tena

iii. Kutoa elimu na kuhamasisha jinsi ya taka zinavyotenganishwa kutokana na alama zilizowekwa kwenye vyombo

**g) Watoa huduma za uzoaji wa taka ngumu**

Watoa huduma ya uzoaji wa taka ngumu watekeleze dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza kwa kufanya yafuatayo:

i. Kutoa elimu ya utenganishaji wa taka kwa jamii na wafanyakazi (zinazooza, zisizooza na hatarishi)

ii. Kuweka vyombo vitatu kwenye maeneo ya muda ya kukusanyia taka

iii. Kusafirisha taka zikiwa zimetenganishwa

iv. Kuhakikisha taka zinazokusanywa katika maeneo mbalimbali zinafikishwa kwenye vituo vya urejelezaji au dampo

# SURA YA TANO

## 5.0 MAJUKUMU YA WASIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Mwongozo huu unatoa maelekezo mahsusi ya namna ya kutekeleza dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza. Katika kutekeleza Mwongozo huu, masuala yafuatayo yazingatiwe:

i. Mamlaka za usimamizi na wazalishaji wa taka ngumu wajumuishe dhana ya PTR katika Bajeti na Mipango yao ya maendeleo.

ii. Kuwepo kwa Mratibu wa mpango wa dhana ya punguza, tumia tena na rejeleza na kuunda Timu ya usimamizi

iii. Kuwepo taarifa ya aina ya taka na hali ya uzalishaji

iv. Kushirikishwa kwa wadau katika Mpango wa dhana ya punguza, tumia tena na rejeleza.

v. Kufanyika Tathmini ya fursa za utekelezaji wa mpango wa dhana ya punguza, tumia tena na rejeleza

vi. Kutekeleza Programu ya dhana ya punguza, tumia tena na rejeleza

vii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kuboresha Programu

## 5.1 Maelekezo mahsusi kwa kila mdau katika kutekeleza Mwongozo huu ni kama ifuatavyo:

### 5.1.1 Wizara yenye dhamana ya kusimamia Mazingira na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

Wizara yenye dhamana ya kusimamia Mazingira itafanya yafuatayo:

i. Kutoa elimu kwa Umma kuhusu utekelezaji wa Mwongozo

ii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mwongozo

### 5.1.2 Wizara yenye dhamana Mamlaka ya Serikali za Mitaa

i. Kuandaa utaratibu kuwezesha upatikanaji wa rasilimali zitakazowezesha utekelezaji wa Mwongozo

ii. Kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa

iii. Kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mwongozo kwenye Wizara yenye dhamana ya mazingira

### 5.1.3 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitafanya yafuatavyo:

***a). Kuhuisha dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza katika Mipango yao kwa kufanya yafuatayo;***

i. Kuandaa utaratibu kuwezesha upatikanaji wa rasilimali zitakazowezesha utekelezaji wa Mwongozo

ii. Kuhamasisha utekelezaji wa mpango wa PTR

iii. Kuingiza vipengele vinavyohusu utekelezaji wa PTR kwenye mikataba yote wanayoingia

iv. Kutenga maeneo la kukusanyia Taka ngumu zinazoweza kurejelezwa katika Kata ambayo yanaweza kuwa kuendeshwa na kusimamiwa na Sekta binafsi, Vikundi vya Kijamii au Mashirika yasiyo ya Kiserikali

v. Kutoa motisha kwa wadau wote wanaonekana kufanya vizuri katika utekelezaji wa mpango wa PTR

***b). Kuratibu utekelezaji wa mpango wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza***

Utekelezaji wa Mpango wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza utaratibiwa na Mkuu wa Idara ya mazingira na udhibiti wa taka ngumu husika kwa kila Halmashauri na kuaandaa taarifa na kuwasilisha Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

***c). Kuandaa taarifa ya aina ya taka na hali ya uzalishaji***

Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae taarifa kuhusu aina, kiasi na chanzo cha taka kinachozalishwa. Rejea Kiambatisho Na. 1 (Taarifa za uzalishaji wa taka ngumu).

Taarifa hizo zitaandaliwa katika ngazi ya Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Mtaa, Kata na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, majukumu yao katika kuandaa taarifa husika ni pamoja na:

i. Ofisi ya Mtendaji wa Mtaa

- Kukusanya taarifa za uzalishaji taka, kiasi kinachokusanywa, watoa huduma, vifaa vinavyotumika

kukusanya na kusafirisha kutoka kwenye maeneo yake ya kiutawala.

- Kukusanya taarifa za wadau wanaojihusisha na shughuli za PTR.
- Kuandaa taarifa na kuwasilisha kwenye Ofisi Mtendaji wa Kata (Rejea Viambatisho Na. 1 na 3)

ii. Ofisi ya Mtendaji wa Kata

- Kuwasilisha dodoso la ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji wa taka katika ngazi ya Mtaa.
- Kuandaa taarifa ya Kata kuhusu uzalishaji taka, kiasi kinachokusanywa, watoa huduma, vifaa vinavyotumika kukusanya na kusafirisha kutoka kwenye maeneo yake ya kiutawala.
- Kuwasilisha taarifa ya Kata kuhusu usimamizi na udhibiti wa taka ngumu na wadau wanaojihusisha na dhana ya PTR kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Taarifa hizo ziwasilishwe kila baada ya miezi mitatu (3).

iii. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa

- Kuwasilisha jedwali la kukusanya taarifa kwenye Ofisi za Watendaji wa Kata kuhusu uzalishaji taka, kiasi kinachokusanywa, watoa huduma, vifaa vinavyotumika kukusanya, kusafirisha na wadau wanaojihusisha na dhana ya PTR. (Rejea Kiambatisho Na.1)
- Kuhamasisha uwepo kwa vifaa vya kuhifadhia taka kwa kila kaya vitakavyotumika kupata taarifa za aina na kiwango cha taka kinachozalishwa katika utekelezaji wa dhana ya PTR.

- Kuhakikisha watendaji wa Kata kuchagua angalau asilimia 5 ya idadi ya Kaya zake kwa ajili ya kutumika kubaini aina za taka na kiwango cha uzalishaji.
- Kuwaelekeza watoa huduma ya uzoaji taka kuchukua taka zilizokusanywa katika kaya na kuzipeleka kwenye eneo lililotengwa.
- Kuandaa taarifa ya hali ya usimamizi na udhibiti wa taka ngumu katika eneo lake la utawala husussan utekelezaji wa dhana ya PTR. Taarifa hizo ziwasilishwe kwenye Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa kila baada ya miezi mitatu (3).

***d). Kuwashirikisha wadau katika kuainisha fursa za utekelezaji wa mpango wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza***

Mamlaka za Serikali za Mitaa zifanye tathmini ya fursa mbalimbali zilizopo katika utekelezaji wa Mpango wa dhana ya PTR ikiwa ni pamoja na kuainisha:

i. Wakusanyaji wa taka zinazoweza kurejelezwa

ii. Viwanda vinavyofanya urejelezaji

iii. Watengenezaji wa mboji

iv. Wanunuzi wa taka zinazoweza kurejelezwa

v. Aina ya taka zinazorejelezwa katika eneo lake

***e). Kuandaa Programu ya utekelezaji wa Mpango wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza***

Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wadau zitaandaa na kutekeleza Mpango wa utekelezaji ambao pamoja na masuala mengine utaainisha masuala yafuatayo:

i. Aina ya taka zinazolengwa Kupunguzwa, Kutumika Tena na Kurejelezwa

ii. Kiwango cha taka kinachokusudiwa kupunguzwa

iii. Kuainisha rasilimali zitakazohitajika katika kutekeleza mpango wa PTR

iv. Makadirio ya gharama zitakazotumika kutekeleza dhana ya PTR

v. Vigezo vya kupima mafanikio ya Mpango

Rejea Kiambatisho Na. 3: Mpango wa Utekelezaji wa PTR

***f). Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kuboresha Programu***

Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa dhana ya punguza, tumia tena na rejeleza ifanyike kila baada ya miezi mitatu (3) kulingana na malengo yaliyowekwa.

### 5.1.4 Viwanda

Viwanda vitatekeleza dhana ya PTR kwa kufanya yafuatayo:

***a). Kuteua Msimamizi wa utekelezaji wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza***

Msimamizi atasimamia utekelezaji wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza taka na kuandaa taarifa ya hali ya uzalishaji wa taka na utekelezaji wa PTR katika kiwanda. Taarifa hiyo ioneshe kiasi cha taka kinachozalishwa, utekelezaji wa dhana ya PTR na utupaji salama wa taka zinazobaki. Rejea Kiambatisho Na. 1 (Taarifa za uzalishaji wa taka ngumu).

### b). *Kuandaa Programu ya utekelezaji wa Mpango wa dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza*

Viwanda vitaandaa na kutekeleza Mpango wa utekelezaji ambao pamoja na masuala mengine utaainisha masuala yafuatayo:

i. Aina ya taka zinazolengwa Kupunguzwa, Kutumika Tena na Kurejelezwa

ii. Kiwango cha taka kinachokusudiwa kupunguzwa

iii. Kuainisha rasilimali zitakazohitajika katika kutekeleza mpango wa PTR

iv. Makadirio ya gharama zitakazotumika kutekeleza dhana ya PTR

v. Vigezo vya kupima mafanikio ya Mpango

Rejea Kiambatisho Na. 3: Mpango wa Utekelezaji wa PT

# SURA YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

Ikumbukwe kuwa kila mwananchi anao wajibu wa kutimiza majukumu yaliyoainishwa katika Mwongozo huu. Aidha, wadau wote wakiwa ni pamoja na wazalishaji wa taka ngumu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, watoa huduma ya uzoaji wa taka na warejelezaji wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa dhana hii kwa usimamizi endelevu wa taka ngumu nchini.

**Kiambatisho Na. I:**

***Jedwali Na. 1: Taarifa za uzalishaji wa taka ngumu***

| Taarifa | Lengo |
|---|---|
| **Idadi ya wakazi, kiasi na aina ya Taka** | Kupata taarifa za kiasi cha taka kinachozalishwa katika kila chanzo (Makazi, ofisi, biashara, taasisi nk.) kwa kila siku; Aina ya taka hizo (plastiki, chuma, karatasi, nk); Shughuli kuu zinazopelekea uzalishaji wa taka hizo; |
| **Aina ya usafiri, Ujazo** | Kupata taarifa za kiasi cha taka kinachokusanywa kulingana na aina mbalimbali ya vyombo vya usafiri |
| **Kiasi cha taka kinachopelekwa dampo** | Kupata taarifa ya idadi ya magari na ujazo wake yanayoingiza taka dampo kila siku |
| **Muda na namna ya ukusanyaji wa Taka** | Kupata taarifa za ratiba ya ukusanyaji taka na namna zinavyoukusanywa (Mf. Nyumba kwa nyumba, sehemu maalum iliyotengwa, nk.) ili kubaini changamoto mbalimbali |
| **Hali ya urejelezaji wa taka ngumu** | Kupata taarifa ya hali ya urejelezaji wa taka unavyofanyika kuanzia ngazi ya uzalishaji mpaka kwenye dampo |
| **Mahitaji ya Mbolea na hali ya soko** | Kupata taarifa ya fursa za uzalishaji wa mbolea na tathmini ya uhitaji wa mbolea hiyo |

**Kiambatisho Na. 2:**

***Jedwali Na. 2: Tarifa za aina ya taka na kiwango kinachozalishwa katika maeneo ya makazi***

| Tarehe | Aina ya Taka | Kiasi (Kg) |
|---|---|---|
| | Taka zinazooza | |
| | Taka za Plastiki | |
| | Nguo | |
| | Majani na Mbao | |
| | Ngozi | |
| | Chuma | |
| | Kioo | |
| | Taka nyingine | |

## Kiambatisho Na. 3

*Jedwali Na. 3: Mpango wa Utekelezaji wa PTR*

| Aina ya Taka | Kiasi cha taka kinachozalishwa kwa mwezi(Kg) | Aina ya PTR (Punguza/ Tumia tena/Re-jeleza) | Shabaha ya kiasi kinacho-lengwa kupun-guzwa (kg) | Muda wa utekeleza-ji | Gharama zilizotumika (TSh) | Hali ya utekelezaji | Mtaalamu/ Msimamizi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

# ORODHA YA NYARAKA ZILIZOREJEWA


1 *International Growth Centre (IGC): (2014). Urbanization in Tanzania. London School of Economic and Political Science.Houghton Street, London WC2A 2AE.*

2 *Kingu, A., and Yhdego, (2016). Solid Waste Management in Urban Centres of Tanzania Leapfroging towards a Circular Economy.*

3 *Omar, H.M. (2019). The Influence of Institutional Factor to the Sustainability of Informal Solid Waste Collectors: The Case of Kinondoni Municipality-Tanzania. In the Global Scientific Journals. Vol.7/ Issue 10/October 2019, Online ISSN 2320-9186*

4 *Omar, H.M. (2020). Assessment of Refuse Collection Charges in covering Waste Management Cost: The Case of Ilala Municipality-Dar es Salaam, Tanzania.*

5 *Omar, H.M. (2021). The Governance Approaches and Their Impact on Solid Waste Collection Perfomance in Selected Local Government Authorities in Tanzania. In the Global Scientific Journals (GSJ). Vol.9/Issues1/ January, 2021. Online: ISSN 2320-9186*

6 *Srinivas, H. (2015).Inspiring Ideas from Japan's 3R Initiatives. Case Study Series E-099.May 2015*

7 *United Republic of Tanzania: (2018). Dar es Salaam Master Plan 2016-2036*

8 *United Republic of Tanzania-Vice President Office: (2019a). Waste Management Investment Guide*

9 *United Republic of Tanzania-Vice President Office: (2019b): Open Burning Inventory Reports.*

10 *Visvanathan, C., Adhikari, R., and Ananth A.P., (2007). 3R Practices for Municipal Solid Waste in Asia. Linnaeus Eco-Tech · December 2007. DOI: 10.15626/Eco-Tech.2007.002*

11 *Waste Atlast (2012). Country Data: Tanzania*